MAOMBI

Ya Kujikuza kiroho

TOLEO LA 4

BY DENIS & DEVIS JULIUS

MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.

~Toleo la nne

UTANGULIZI:

Huu ni mwendelezo wa mwongozo wa maombi maalumu ya kujikuza kiroho. Ikiwa hujapata mwongozo wa nyuma basi unaweza kuwasiliana nasi kwa namba zilizo chini ya makala hii ili tuweze kukutumia.

Ni mwongozo wa maombi ya siku saba (7), ambapo tunakuwa na SAA 6, za maombi, kuombea vipengele hivyo muhimu ambavyo vinahusiana na moja kwa moja sisi kukua kwetu kiroho. Kumbuka Mungu humpa mtu kile amwombacho. Huwezi kumwomba mkate akampa samaki. Ikiwa maombi yako sikuzote ni kumlilia Mungu akupe gari, sahau Mungu kukupa upako.

Wakristo wengi ni waombaji, lakini wanakosa shabaha ya vitu muhimu vya kuomba. Na ndio hapo tunaomba vitu vile vya ziada, tunasahau vile vya msingi ambavyo ndio vingeleta vya ziada baadaye. Sulemani alimwomba Mungu hekima, lakini hekima ilileta mali baadaye. Kwasababu alijua ni nini ambacho anapaswa aombe kwa Mungu wake.

Utaona labda ni mkristo amekaa katika wokovu miaka 20, lakini kiroho ni mchanga kama mwongofu aliyeokoka mwezi mmoja nyuma. Utajiuliza ni kwanini? Ni kwasababu hajaelekeza nguvu zake nyingi katika eneo la ukuaji, Bali katika mambo mengi ambayo kimsingi hayamjengi, yanajenga vitu vyake

Hivyo mwongozo huu utakusaidia kukuimarisha kama sio kupanua wigo wako wa kimaombi. Na kama ukizingatia kutumia muda wa saa hizo 6 katika wiki yako yenye siku saba, kuombea mambo hayo, basi utaanza kupiga hatua kubwa sana kiroho. Mungu mwenyewe atahusika kukupanua kiufahamu rohoni.

Vilevile ukuaji hutegemea na kujifunza pia Neno la Mungu, Hivyo ikiwa utapenda uwe unapata mafundisho ya biblia kila siku basi waweza tembelea tovuti yetu hii www.wingulamashahidi.org, utakutana na masomo zaidi ya 4,000, Au wasiliana nasi kwa namba zilizo chini ya chapisho hili, tukuweke katika orodha ya watakayokuwa wanayapokea kwa njia ya simu.

Karibu sasa katika mwongozo wetu mpya..

~Mwl Denis & Devis Julius

KIMO CHA MTU MKAMILIFU:

(2Petro 1:1-11)

2Petro 1:8 Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.

Mtume Petro, alitambua umuhimu wa mkristo yoyote kukua kiroho. Hivyo katika moja ya nyaraka zake, akaeleza mambo ya msingi ambayo kila mwaminio anatakiwa awe nayo ndani yake. Tuyasome.

2Petro 1:5 Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, 6 na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, 7 na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. 8 Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.

Utaona hapo ametanguliza kwa kusema "katika imani yenu". Akiwa na maana katika wokovu wako ulioupata ongezea, mambo yafuatayo ili mambo yawe sawa.

1. **WEMA**
2. **MAARIFA**
3. **KIASI**
4. **SABURI**
5. **UTAUWA**
6. **UPENDANO WA NDUGU**
7. **UPENDO**

Tukishajua yana faida basi Nasi hatuna budi kuyaombea, ili Bwana atusaidie yatoke ndani yetu sawasawa na atakavyo yeye. Kwasababu tusipoyaombea, si rahisi kuyatenda, tutabakia kuyatamani tu lakini yasiwe dhahiri maishani mwetu.

1) **WEMA** (dk50)

Wema ni kitendo cha kuonyesha kujali, kuthamini, nidhamu na uaminifu. Ni Moja ya matunda 9 ya Roho (Wagalatia 5:22). Lakini je wema wetu tuonyeshe kwa nani?

- **Kwa wanaotupenda na wasiotupenda:**

Ni rahisi kurudisha wema kwa aliyekuonyesha wema, lakini si rahisi kutenda wema kwa anayekuchukia, au adui yako. Lakini Bwana ataka tuwe wema kwao tuwasaidie pia kwasababu yeye naye huwapa mvua yake waovu na wema.

- **<u>Kwa tunaotumika nao:</u>**

Kama wewe umeajiri watu, si lazima umlipe mfanyakazi wako mshahara ule ule tu, waweza pia kumwongozea posho. Huo ndio wema hasaa, kumpa kitu ambacho hakustahili. Yesu alitoa mfano ule wa Yule mwajiri aliyewalipa wafanyakazi mishahara ambayo hawajafanya kazi sana sawa na wale wengine. Lakini wale waliopewa sana wakakasirika kwasababu wenzao walilipwa sawa na wao, Yesu akasema..

Mathayo 20:15 "Si halali yangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au jicho lako limekuwa ovu kwa sababu ya mimi kuwa mwema?

Si lazima iwe kwenye ngazi ya mwajiri, na wewe, pia uliyeajiriwa, waweza kufanya kazi ya ziada, ambayo ipo nje ya mshahara wako, huo ndio wema, Halikadhalika mpaka kwenye eneo la kihuduma na kikanisa. hapo Bwana atakuona umekomaa kiroho. Hivyo ombea vipengele hivi;

- ✓ Mwombe Bwana wema wako usiwe na mipaka, uufikie mpaka wasiokupenda
- ✓ Mwombe Bwana akupe moyo wa kufanya zaidi ya malipo uliyostahili popote ulipo
- ✓ Bwana akupe kuwajali wengine wenye shida. Mfano wa Yule msamaria
- ✓ Bwana akupe kuwatendea wema watumishi wote wanaotenda kazi katika shamba la Mungu
- ✓ Bwana akupe kuvitendea wema pia viumbe vyake alivyoviumba
- ✓ Bwana akupe kuwatendea mema wanaokutegemea, na unaowategemea
- ✓ Bwana akupe kuwatendea mema ndugu zako na jamaa zako wa karibu.
- ✓ Bwana akupe moyo wa kulitendea wema taifa lako.

2) <u>MAARIFA</u> (dk50)

Bwana anasema watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa. Tukosapo maarifa tunakosa shabaha ya mambo mengi, ikiwemo kumwelewa Mungu mwenyewe. Wayahudi walipingana na mitume na Bwana, ikawafanya mpaka juhudi yao ya kumtafuta Mungu ikawa ni bure kwasababu tu walikosa maarifa (Warumi 10:2). Hivyo..

- ✓ Omba Bwana akupe moyo wa kupenda kusoma sana Biblia pamoja na vitabu vya kiroho. Kama Danieli, ili uweze kuongeza wigo wako wa kiuelewa
- ✓ Omba Bwana apanue wigo wako wa kuyaelewa maandiko.
- ✓ Omba Bwana akukutanishe ni mafundisho sahihi yenye kukujenga.
- ✓ Omba Mungu akupe kuitambua sauti yake inayosema nawe kwa wakati huu.
- ✓ Omba Bwana akupe kuitambua kweli yote ili uwe huru.
- ✓ Bwana atanue eneo lako la kifikra, na kiundaji kazi rohoni.
- ✓ Omba Mungu akuepushe na mafundisho ya mashetani na manabii wa uongo

3) KIASI (dk50)

Kiasi ni ule uwezo wa kudhibiti jambo/tendo lisipitilize mipaka yake, yaani litendeke kwa sehemu tu. Kiasi ni moja ya tunda la Roho (Wagalatia 5:22). Kumbuka kuwa Mambo mengi ya mwili yasiyokuwa na madhara kwetu rohoni Bwana ametutaka tuwe nayo na kiasi ili tuweze kupata muda wa kuwa faragha na yeye;

Haya ni maeneo ambayo Bwana anataka tuwe na kiasi nayo; Hivyo ombea.

- **Kiasi katika shughuli za ulimwengu**

  1Wakorintho 7:31 Na wale wautumiao ulimwengu huu, kama hawautumii sana; kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita. 7.32 Lakini nataka msiwe na masumbufu. Yeye asiyeoa hujishughulisha na mambo ya Bwana, ampendezeje Bwana;

  - ✓ Omba Bwana akupe kiasi katika shughuli zako, ili usiwe ili mbegu iliyoangukia kwenye miimba ikasongwa katika shughuli za ulimwengu, ikawa haizai.(Marko 4:19)

- **Kiasi katika kuzungumza:**

Mithali 10:19 Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu; Bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili

- ✓ Mwombe Bwana akuponye kinywa chako. Uwe mwepesi wa kusikia lakini sio kunena

- **Kiasi katika ndoa**

Ikiwa wewe ni mwanandoa, Bwana anataka uwe na kiasi kwenye eneo lako la tendo. Ili upate muda wa kumtafakari yeye, lakini pia shetani asipate nafasi ya kuwajaribu. (1Wakorintho 7:4-5)

- ✓ Omba Bwana akupe nia ya kiasi kwenye ndoa yako

- **Kiasi katika huduma:**

Sio kwamba uwe na kiasi kumtumikia Mungu hapana. Bali nia ya kiasi, yaani usitake wewe ufanye kila kitu mwenyewe. Au wewe ndio uwe na karama zote duniani. Bali kwa kile kipimo ulichowekewa na Mungu ufanye (Soma Warumi 12:3-5)

- ✓ Mwambie Bwana akupe kutazama kile alichokiweka ndani yako ukikuze, umtumikie kwa bidii, mengine atende yeye.

- **Kiasi katika mwenendo:**

Maandiko yanaagazia vijana wawe na mwenendo wa kiasi, vilevile wazee na wanawake. Mfano Katika eneo la uvaaji, na tabia (1Timotheo 2:9, 3:11, Tito 2:6).

- ✓ Mwambie Bwana nisipitilize staha, mwenendo wangu uonekane kama vile ni mtu niliyezaliwa na Kristo.

- **<u>Kiasi katika Haki:</u>**

Ukisoma Mhubiri 7:16, Mungu anakataza watu kujihesabia haki, kupita kiasi, yaani kujiona wewe ni mtakatifu mbele za Mungu kuwazidi wengine. Mfano wa Yule Farisayo aliyekwenda kuomba hekaluni, akamdharau Yule mtoza ushuru. Matokeo yake ikawa ni mtoza ushuru kuhesabiwa amestahili kuliko yeye.

- ✓ Omba Bwana akupe unyenyekevu, na kujiona wewe si kitu mbele za Mungu zaidi ya wengine.

4) <u>SABURI</u> (dk50)

Saburi ni ile hali ya uvumilivu , kukubali kusubiri hata katika kipindi cha mateso au masumbufu, kwa ajili ya Mungu.

Warumi 5:3 Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; 4 na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini;

- ✓ Omba Bwana akupe saburi katika utumishi aliokuweka
- ✓ Akupe Saburi Katika kumngojea Bwana (Kurudi kwake)
- ✓ Saburi Katika kuzisubiria ahadi za Mungu. Mfano wa Ibrahimu
- ✓ Saburi Katika Kuomba
- ✓ Saburi katika kutenda haki. Mfano wa Ayubu.

5) <u>UTAUWA</u> (dk50)

Utauwa ni Utakatifu. Mungu anataka sote tuwe watakatifu kama yeye alivyo. Makerubi mbinguni walipomtazama Mungu hawakuona kingine zaidi ya utakatifu. Vivyo hivyo na sisi hatuna budi kufanana na yeye katika eneo hili.

1Petro 1:16 kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu.

- ✓ Mwombe Bwana akujalie neema ya ‘kupenda’ kuishi maisha matakatifu

- ✓ Akupe kuiona dhambi na uikwepe
- ✓ Akuepushe na watu au mazingira yatakayokupelekea kumkosea Bwana
- ✓ Amekee shetani asikwe kikwazo kwako
- ✓ Akuepushe na tamaa ya macho na ya kuupenda ulimwengu.
- ✓ Akujalie kulitunza hekalu lake (mwili wako)
- ✓ Akupe moyo safi na wa ibada.

6) UPENDANO WA NDUGU. (dk50)

Sisi kwa sisi (Tuliokoka), tumepewa amri ya kupendana. (Yohana 15:12). Hivyo huna budi kuhakikisha jambo hili linatoka ndani yako kwa msaada wa maombi.

- ✓ Omba Bwana akupe kumpenda jirani yako kama nafsi yako
- ✓ Omba Bwana akupe moyo wa kuachilia na kusamehe haraka
- ✓ Omba Mungu akupe neema ya kujali shida za wengine
- ✓ Omba Bwana akupe kupenda umoja na wenzako
- ✓ Mwambie Bwana akuondolee ubinafsi
- ✓ Afukuzie mbali roho ya wivu na mashindano ndani yako
- ✓ Bwana akujalie kuwa tayari kutoa ulivyo navyo kwa ajili ya ndugu zako,

7) UPENDO (dk50)

Hichi ndio kilele cha juu kabisa cha ukamilifu wa mwanadamu yoyote, ndicho ambacho Mungu anatazamia sote tufikie. Kwasababu yeye ndio Upendo wenyewe. Upendo huu ni tofauti na ule upendano wa ndugu, ambao unaosababu. Huu hauna sababu, unapenda bila masharti, ndio ule wa kuwapenda maadui zako, na kuwaombea, kupenda kila kitu, kujitoa kikamilifu kwa wengine. Ndio unaozungumziwa katika 1Wakorintho 13. Hivyo..

- ✓ Omba Bwana akupe kumpenda yeye, kwa moyo wako wote, roho yako yote, akili zako zote,a na nguvu zako zote katika Roho na kweli
- ✓ Bwana akupe kujitoa kwake, kwa hali zote. Kumtumikia kwa auminifu
- ✓ Omba Bwana akupe kuwapenda wasiokujali/maadui zako
- ✓ Omba Bwana akupe moyo wa kuwaombea wanaokuudhi.
- ✓ Omba Bwana akupe kupenda viumbe vya asili na dunia yake
- ✓ Omba akupe kuwapenda watu wengine kama nafsi yako
- ✓ Bwana akupe kuvumilia yote
- ✓ Kustahimili yote,
- ✓ Kutohesabu mabaya,
- ✓ Kutoona uchungu
- ✓ Kutoonea wengine wivu,

- ✓ Kukataa kujivuna na kujidai

Tukiomba kwa bidii juu mambo hayo. Kama vifungu hivyo vinavyotuhimiza mishoni kwamba tutakuwa watu ambao “tuna matunda” na “sio wavivu”. Maana yake ni kuwa uwepo wako duniani kama mtakatifu utadhihirika, na ile nuru Mungu aliyoiweka ndani yako itatokea, na utakuwa mtu wa kupanda daraja jipya kila siku. Hakikisha unachukua muda wa dakika 50, kuombea kila kipengele.

Bwana akubariki sana.

Usikose mwendelezo...

Bwana akubariki.

Kwa ushauri/ Msaada/ Maombezi wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312